**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA,**
**S.L.P.1405,**
**IRINGA.**
____/____/_____.

**KUMB. NA.IDC/ FSS/2427/FOJI/ /01**

Mkuu wa shule: **DAVID ELIA KYANDO.**
Simu no. **0717657802/0752183065**
Makamu mkuu wa shule: **JUMA HONORATUS LWEHELA.**
Simu no**. 0713578808/0759784947**
E-mail: furahiasss2467@gmail.com.

---

**MZAZI/MLEZI WA**
**…………………………………………………………………**
**S.L.P………………………………………………………..**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI FURAHIA, HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, MKOA WA IRINGA MWAKA .......**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii kwa mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya **HGL, HKL** na **HGK.** Shule ina kidato cha kwanza mpaka cha sita ambapo kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne ni mchanganyiko na kidato cha tano na sita ni wavulana.

Shule ya Sekondari Furahia ipo umbali wa Kilometa 70 kutoka Iringa mjini katika Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa, kijiji cha Usolanga, kata ya Malengamakali**. Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana stendi kuu ya zamani **Iringa mjini** kwa nauli ya Shilingi 6000/=. Ukifika stendi kuu ya zamani panda basi la kwenda **Nyakavangala.** Basi la abiria linalofika shule moja kwa moja huondoka stendi ya zamani Iringa mjini saa **7:30 mchana**, hivyo unashauriwa kuwahi kufika stendi kabla ya muda huo ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.
Muhula wa Masomo utaanza tarehe **................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ................................

***NINAKUKARIBISHA SANA.***

**…………………………………**

**DAVID ELIA KYANDO**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA**

**A: MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE.**

F.01

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA,**
**S.L.P.1405,**
**IRINGA.**

**1. SARE ZA SHULE**

i. Suruali mbili za rangi ya dark blue ndefu na zisizobana mwili.
ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
iii. Sweta rangi ya kijivu **(shingo V)**
iv. Sare ya Michezo ni **Bukta na T-shirt za blue (za Taifa stars) na raba za michezo.**
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; **(Jozi mbili na kuendelea)**
vi. Soksi ndefu nyeupe **(Jozi mbili na kuendelea).**
vii. Track suit rangi ya light blue **(sweta lisilo na kofia).**
viii. Shamba dress ni suruali ya damu ya mzee **(maroon)** na tisheti nyeusi yenye kola na mistari myeupe begeni na mikononi.
ix. T-shirt ya shule mwanafunzi atapewa mara afikapo shuleni kwa gharama ya Tsh. 12,000/=.

**NB. Kwa wale wenye matatizo ya kiafya mfano kifua au pumu waje na puluneki nyeupe**.

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:**

i. Madaftari (*counterbook kuanzia kumi*)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka; (moja kwa kila muhula)
iii. Godoro futi 2 kwa inchi 2 na nusu
iv. Mafaili mawili (Spring file za plastic). Kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu muhimu za mwanafunzi.(Yanapatikana shuleni kwa sh. 5000/= yote mawili)
v. Brash ngumu moja na brush laini moja yenye mpini mrefu kwa ajili ya usafi.
i. Mashuka Jozi 2 (rangi ya pinki na blue), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
ii. Nguo za ndani za kutosha;
iii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
iv. Ndoo 2 (moja lita Kumi na nyingine lita ishirini) zenye mifuniko;
v. Begi la daftari.
vi. Toilet paper.
vii. Mahitaji mengine ya kutosha kama sabuni, mswaki, dawa ya meno, rangi ya viatu, brashi ya viatu na mafuta ya kujipaka.
viii. Tochi moja ya betri au ya solar itakayotumika kukiwa na tatizo la umeme.
ix. Kamusi ya kingereza (Dictionary).
xi. Matokeo ya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne (Result slip)

xii. Vifaa vya kujanavyo kwa kila tahasusi tahasusi.

| TAHASUSI | MAHITAJI |
|---|---|
| HGL | Panga moja. |
| HGK | Shoka moja lenye mpini. |
| HKL | Jembe moja lenye mpini. |

## 1.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

**Mchango wa bima ya Afya shillingi ni 50,400/= kwa mwaka hii ni kwa wale ambao hawana bima ya afya.**

Malipo yafanyike kupitia akaunti namba 60501100097 NMB jina la akaunti ni Furahia Secondary school na unapokuja shuleni uje na stakabadhi ya benki (Bank Pay Slip).

***NINAKUKARIBISHA SANA.***

**……………………………….**

**DAVID ELIA KYANDO**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA**

## B: FOMU YA SHERIA NA KANUNUNI ZA SHULE.

F.02

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA,**
**S.LP.1405,**
**IRINGA.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2. MWANAFUNZI ANAPASWA KUFUATA NA KUTEKELEZA SHERIA NA KANUNI ZIFUATAZO;

#### 2.1 *MAHUDHURIO.*

1. Kuthamini muda wa kuwepo mahali anapotakiwa kwa mujibu wa taratibu za shule au maelekezo kutoka uongozi wa shule.
2. Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini asubuhi
3. Kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa unapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mwalimu wa darasa/zamu / mkuu wa shule.
4. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo bila kukosa mafundisho ya dini kwa mujibu wa dhehebu lako.(Ijumaa/Jumamosi /Jumapili).
5. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku ( Night Preparation ).
6. Kuhudhuria mikutano halali ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa uasafi na mikutano ya kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa.
7. Kuitikia miito ya dharura mara moja.
8. Kutotoka nje bila ya ruhusa.

#### *2.2 HESHIMA.*

1. Mwanafunzi anatakiwa kusalimia mwalimu au mtu yeyote anaye mzidi umri anapoingia darasani.
2. Mwanafunzi atumie lugha nzuri wakati wote.
3. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi.
4. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
5. Kuitikia mara moja wito wa kengele.
6. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa vyama na serikali, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
7. Kuheshimu taratibu za mkutano, ofisi za shule mali binafsi na mali ya Umma.
8. Kusimama kwenye mstari wakati wa kupokea huduma.
9. Kukaa kimya darasani, kutoka nje kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.
10. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na nje ya shule.

11. Kuwaheshimu walimu na wafanyakazi wasio walimu.
12. **Baadhi ya tabia ambazo hauruhusiwi mwanafunzi:**
    A. Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya na pombe.
    B. Kufuga; kucha na nywele ndefu, ndevu na kupaka rangi kwenye nywele au kucha
    C. Kuvaa mavazi yasiyo kuwa na heshima.
    D. Kugombana, kupigana, kutukana nk.
    E. Uasherati, wizi, utapeli.
    F. Imani za kishirikina.
    G. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

## 2.3 *SARE ZA SHULE*

Sare ya shule itavaliwa wakati wa;

a) Masomo darasani
b) Unapotoka nje ya shule kwa shughuli za shule
c) Mhadhara wa shule (school baraza)
d) Unapokwenda hospitalini
e) Maandamano halali.
f) Wanafunzi wanaposafiri kuja shule au kwenda kwao wakati wa likizo
g) Wanafunzi wawe na nguo za kazi za mikono (Shamba dress) wakati wa kazi za nje ya darasa.
h) Wanafunzi wawe na nguo za michezo.
i) Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo haviruhusiwi
j) Nguo ziwe safi wakati wote
k) Lazima kuwa na kitambulisho.
l) Kuvaa sare ya kushindia wakati husika.
m) Ni marufuku kuhudhuria minadani/gulio ukiwa shule isipokuwa kwa kibali maalum kutoka kwa mkuu wa shule.

## 2.4 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE;

1. Wizi.
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga/Usagaji.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji wa bangi na sigara.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendera.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
11. Kutoa mimba/kushawishi kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu ndani au nje ya shule
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoka nje ya kijiji hiki bila ruhusa ya maandishi toka kwa mkuu wa shule.
15. Kumiliki simu na vifaa vinavyohusiana na simu kinyume na taratibu za shule.
16. Kutoroka bwenini wakati wowote ule au kulala nje ya bweni siku moja au Zaidi bila ruhusa.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Tunza vizuri na kwa usalama fomu hii ije katika hali ya usafi.**

**Ni matumaini yangu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima. Vile vile mwanao atambue kuwa kama hatojituma katika masomo na kupelekea kupata daraja la nne na sifuri kwenye mitihani yake yoyote ile itakayotolewa shuleni, hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake.**

- **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo: -**

- **Mkuu wa shule –0717657802 / 0752183065.**
- **Makamu Mkuu wa Shule – 0713578808 / 0759784947**
- **Mwandamizi Taaluma – 0713929289 / 0757618920.**

*NINAKUKARIBISHA SANA.*

……………………………….
**DAVID ELIA KYANDO**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA**

**C. MEDICAL EXAMINATION FORM**

F.03

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REAGIONAL ADMINISTRATION AND**
**LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY**
**IRINGA DISTRICT COUNCIL**

**FURAHIA SECONDARY SCHOOL,**
**P. O. BOX 1405,**
**IRINGA – TANZANIA**

**To be completed by medical officer in respect of all form(ijazwe na mganga/mhudumu wa hospitali au kituo cha afya kinachotambulika na seerikali)**

FULL NAME ..........................................................................................................................
AGE ..........................................................................................................................
BLOOD COUNT (RED AND WHITE) .........................................................................................
STOOL EXAMINATION.........................................................................................................
URINE ANALYSIS ...............................................................................................................
SYPHILIS TEST ..................................................................................................................
U.P.T..........................................................................................................
EYE TEST ..........................................................................................................................
T.B ..........................................................................................................................
EAR ..........................................................................................................................
CHEST ..........................................................................................................................
SPLEEN ..........................................................................................................................
ABDOMEN ..........................................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical or chronicle of family diseases.**
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................
.....................................................................................................................................

I certify that the above named is fit/not fit to pursue studies with reference to the above comments.
Signature...............................................................................
Designation...........................................................................
Section..................................................................................
Date ..............................

OFFICIAL STAMP

**N.B**

Each student must bring this complete form when coming to school, a student is not going to be enrolled without this certificate of physical fitness.

**D. FOMU YA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI.**

**F-04**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA,**
**S. L.P 1405,**
**IRINGA.**

**TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

1. Jina la mawanafunzi ............................................................. Jinsia: ME ☐ KE ☐
2. Tarehe ya kuzaliwa:
   (**Jaza namba mojamoja kwenye kila kisanduku**)

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2 | 0 | 2 | 6 |

3. Uraia ...................................................... Kabila ..............................................................
4. Shule ya sekondari utokayo ………………………………………………………………
5. Kidato alichopokelewa ............................................. Tarehe ...............................................
6. Jina la baba ..............................................................................................................
7. Jina la mama ..............................................................................................................
8. Anuani ya mzazi au mlezi **S.L.P** .........................................., ..................................................
9. Namba za simu ya mzazi au mlezi ..........................................., .........................................
10. Kazi ya mzazi au mlezi ....................................................................................
11. Wazazi wanaishi pamoja: Ndiyo ☐ Hapana ☐

***NINAKUKARIBISHA SANA.***

………………………………….

**DAVID ELIA KYANDO**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA**

**E. FOMU YA KUKUBALI /KUTAA NAFASI YA SHULE**

F-05

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI FURAHIA,**
**S. L.P 1405,**
**<u>IRINGA</u>.**

***AHADI / KIAPO CHA MWANAFUNZI***

Mimi........................................................................... (mwanafunzi) ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI FURAHIA KIDATO CHA TANO mwaka 2026 kutoka shule ya sekondari.........................................................................., ninaipokea na kuikubali/kutoikubali nafasi niliyo pewa kwa madhumuni ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yangu binafsi na malengo ya taifa.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na jamii inayonizunguka. Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa , familia, jamii na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yote.
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na nyingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapa shuleni ikiwemo utoro wa vipindi darasani.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, nitakubali kurudishwa nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu au kufukuzwa shule pale inapobidi.

................................ ......./....... /.......
Saini ya mwanafunzi Tarehe

***SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI***

Mimi ..........................................................................................(ambaye ni mzazi/mlezi), nakubali au sikubali mtoto wangu (Jina). ........................................................................kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Furahia mwaka 2026.Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule hii. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.

Pia naahidi kumtimizia mahitaji yote mwanangu kama nilivyosoma na kuelewa maelekezo yote.
Anuani yangu ya kudumu ni S.L. P ......................................................, namba ya simu ...................................
Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi au anuani nitaijulisha shule kwa maandishi.

................................... ....../. ...... /..........
Saini ya Mzazi/Mlezi Tarehe

**AHSANTE**